




HADITHI YA MBOZA NA JOGOO



Mtunzi: Upendo Maria
Mchoraji: Matson Chagulilo




Ilikuwa ni wakati wa likizo. Mboza alisafiri na wazazi wake kwenda kumsalimia bibi yake kijijini. Mboza alikuwa na shauku kubwa ya kumtembelea bibi yake. Kila wakati Mboza anapomtembelea bibi yake, bibi humpa zawadi maalum. Sijui wakati huu atapewa zawadi gani.






Walipowasili, walimkuta bibi kituo cha basi
akiwasubiri. Aliwalaki kwa furaha. Mboza alisubiri
kwa hamu kujua bibi atampa zawadi gani.
Alishindwa kusubiri, alimuuliza bibi yake, bibi ni
zawadi gani sasa utanipa? Bibi akamwambia awe
na subira kidogo hadi wafike nyumbani.





Walipofika nyumbani
bibi alitabasamu
kisha alisema, "Kipindi hiki
sijakuandalia zawadi, utajipa
zawadi mwenyewe. Nenda
kamkimbize kuku ukimpata ni
wako."
Bibi alimuonesha
Mboza Jogoo.





Mbio zilianza za kumfukuza Jogoo. Loo! Jogoo
alikimbia kwa kasi zaidi ya Mboza. Mboza
alianguka kwa kishindo puu! Familia yote ilicheka.
Jogoo alikimbia zaidi.






Mboza aliamka na kuanza kukimbia
tena. Jogoo alikimbilia kwenye
kichaka chenye miiba.





“Mboza ni lazima umkamate Jogoo!”
bibi alisema.





Mboza alichukua fimbo.
“Koo! Koo!” alisema Jogoo huku
akijificha zaidi kichakani.


Mboza alimfukuza shii! shii! “Toka sasa na uanze
kukimbia, ewe Jogoo mjanja, nitakukamata tu,”
alisema Mboza.






Jogoo alipoona
fimbo ya Mboza alirukia kwenye mti
wa mwembe uliokuwa karibu.





Mboza alipomuonā jogoo
juu ya mwembe nae aliamua
kupanda kwenye mti wa
mwembe akamkamatie
huko huko. “Koo! Koo!
Koo!” alisema Jogoo.



Tii! Tii! Aligusa gusa
maembe. Maembe
yalidondoka na kumgonga
Mboza kichwani, tii! tii!
Mamaa Jogoo anaangusha
maembe yananigonga
kichwani.



Mboza hakuweza kupanda
tena mwembe ule, aliogopa
maembe yangemdondokea
kichwani. “Koo! Koo!”
Jogoo alisema kwa furaha
akiwa juu ya mti. Alijua
yuko salama. Mboza
alimwangalia huku akiwaza,
“Nitamkamataje Jogoo
huyu?”






“Nitakukamata tu!” Mboza alimwambia
Jogoo. Mboza amepata mbinu
nyingine. “Nitapanda kwenye mti na
hivi vilemba vya bibi.” Alisema Mboza
huku akianua vilemba vya bibi kwenye
kamba.







Mboza aliviunganisha vilemba vya bibi.
Alitengeneza kamba ndefu na imara. Mboza
aliitumia kamba ile kupanda nayo kwenye mti
wa mwembe.





“Koo! Koo!” alisema
Jogoo. Mboza
alipeperusha kamba
ile. Waah! ilitoa sauti
huku ikimsogelea Jogoo.
Jogoo aliogopa
mlio wa kamba.






“Koo! Koo!” Jogoo alilia huku akiruka
kuelekea chini ya mwembe. Mboza nae
huyoo! Akaruka pamoja na Jogoo.





“Bibi,” Mboza aliita. “Nimemkamata Jogoo!

Nifanyeje sasa?”

“Sasa tunaweza kumchinja na kupika chakula
kitamu,” alisema bibi.









“Hatutamchinja leo,” Mboza alisema.

“Nataka kumpa nafasi Jogoo akimbie, nami
nimkimbize tena kesho!”





Familia yote walicheka.